

Dr. Ed Laymance & Natalie Bartoo

Translated into Swahili by:

Eveline Msemu

MIMI NI MTOTO WA MFALME.

Yesu Kristo ni mwana wa Mungu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu akafufuka kutoka kwa wafu, akashinda kifo! Nilipomuomba anisamehe dhambi zangu na kuwa kiongozi wa Maisha yangu, Alisema ndio! Na sasa ni Bwana na Mwokozi wangu!

KWA SABABU HIYO:

Mimi ni mtoto wa Mfalme wa kweli mmoja. Hii inanifanya mimi kuwa mkuu/malkia kwenye ufalme wa Mungu! Mimi ni sehemu ya familia ya Mungu na nina makao ya milele mbinguni- katika kiti cha enzi upande wa kuume wa Yesu. Mungu ameniinua!!! Amenichagua mimi, ananihitaji mimi, na anajali kuhusu mimi. (Ufunuo wa Yohana 1:9; Yohana 1:12; Waefeso 2:6; Waefeso 2:19; 1Petro 2:9; Yohana 14:1-6)

Ninapendwa na Mungu haijalishi kitu chochote – na hiyo haitabadilika kabisa!

(Warumi 5:6-8; 1 Yohana 4:10)

Mimi ni mtoto wa Mungu: Ananipenda, hata wakati ninapofanya maamuzi mabaya. Wakati wote anahitaji mambo mazuri kwa ajili yangu. Wakati wote. (1Petro 2:9; 1Wakorintho 6:19; 1Yohana 5:11-13; Yohana 3:16; Warumi 5:9; Waefeso 1:13-14)

Mimi ni mkristo. Ninamwili huu huu lakini utu wangu wa ndani nimebadilika. Nina utambulisho mpya – Mimi ni mtoto wa mfalme!

(1Petro 4:16; 2Wakorintho 5:17; Wagalatia 2:20)

Mimi ni nyumba ambayo Mungu anaishi! Na hiyo inanifanya mimi kuwa wa pekee sana. Anatembea na mimi kila mahali ninapokwenda, ananisaidia kufanya maamuzi sahihi na ananionyesha namna/njia sahihi ya kuishi. (Waefeso 2:22; 1Wakorintho 6:19)

Ninaweza kuongea na Mungu wakati wowote, mahali popote, kwa sababu yoyote. Ninaweza kumwambia kila kitu na kumuuliza kitu chochote. Ananisikiliza wakati wote.

(Waefeso 2:18; Wafilipi 4:6-7)

Mimi ni kiumbe kizuri cha Mungu! Ameniumba kwa mikono yake na anampango mzuri na mimi, hivyo kila uamuzi ninaoufanya unamaana. (Zaburi 139; Waefeso 2:10; Wakolosai 1:16; Wagalatia 6:7-9)

Siogopi kifo kwasababu najua kwamba siku hiyo ikifika, nitapata kuishi mbinguni na Mungu milele!

(Warumi 6:8-11; Waebrania 2:14-15; Yohana 14:1-6)

Nimesamehewa kila dhambi niliyowahikuifanya na nitakayoifanya- kabisa 100%, njia zote hakuna kurudi nyuma, haijalishi chochocte!!! (1Yohana 1:9; Zaburi 103:8-13)

Ninafurahia nikiwa na Mungu, kwenye mwanga wake, kilasiku, sasa na siku zote. Woah!

(Warumi 3:23, 6:16-23; Yohana 3:16; 1Peter 1:3; Waefeso 2:4-5; Wakolosai 1:13; Wagalatia 5:1)

Sitaacha shetani aninyanyase mimi! Shetani ni adui wa Mungu na hiyo inafanya shetani awe adui wangu. Mungu ni mkuu, Shupavu, Makini, Mwenye Nguvu Zaidi na ni MKUU kuliko shetani! Mungu yuko upande WANGU. (Ezekieli 28: 12-19; Isaya 40: 28-31; 1Petro 5:8; Waefeso 6:10-18; Yakobo 4:7; 1Yohana 4:4)

Mungu ananipenda na yuko kwa ajili yangu, hivyo haijalishi ni nini kitatokea, hakuna kitakacho niweka mbali na Mungu na upendo wake kwangu. Hakuna-

siyo magonjwa, maumivu, hasara, matatizo au huzuni;

siyo unyanyasaji, shida, njaa, vitu vigumu au vinavyoogopesha;

siyo wakati wa kukataliwa, kuachwa au kusahauliwa;

siyo wakati wa maumivu, kuumizwa au ninaotaka kuumizwa;

siyo marafiki, familia au mtu yoyote aliyekinyume na mimi;

siyo vitu ninavyofanya vibaya au vitu watu wanavyofanya vibaya;

siyo Maisha au kifo, Malaika au mapepo;

siyo mambo yaliyopita hali ya sasa au nitakayo yachagua mbeleni au hali yoyote;

Hakuna nguvu, hukuna mtu , hakuna sehemu, siyo kitu chochote kwenye uumbaji wote;

siyo hata shetani mwenyewe anaweza kunitenga na Mungu na upendo wake kwangu!

(Warumi 8:31-39; Waefeso 1:18-23; Wakolosai 2:15)

Niko mikononi mwa Yesu, kwenye mikono ya Mungu, na hakuna anayeweza kunitoa mikononi mwa Mungu. (Yohana 10 27-28)

Sitaogopa shetani na uovu wake kwa sababu Mungu yuko na mimi siku zote, na ameahidi hataniacha wala hatanisahau. Mungu yupo Pamoja na mimi kila mahali ninapokwenda na ananiangalia sikuzote na milele. (Zaburi 23:4, 2Timotheo1:7; Waebrania 13:5; Zaburi 139:7; Mathayo 28:19-20)

Mimi ni mtoto wa Mfalme – Mungu wa Kweli Mmoja – na leo,

Ninachagua kuishi kwa namna hiyo!